

**Jibu:** Turejee.

*Mithali 20:1 “Mvinyo hudhihakiki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima”.*

Hili ni andiko linaloelezea mambo makuu mawili yanayowakosesha watu waliopungukiwa na Hekima.. na Mambo hayo ni “**Mvinyo**” pamoja na “**Kileo**”. Na vitu vyote hivi viwili vina madhara kwa mtu anayevitumia..

**Sasa ni ipi tofauti kati ya Mvinyo na Kileo? Na madhara yake ni yapi kwa mtumiaji?.**

“**Mvinyo**” (kwa lugha ya kiingereza ni “wine”) ni kilevi kinachotengenezwa kwa “**Matunda yaliyosagwa**” kama Zabibu, mananasi, maembe n.k Mfano wa mvinyo unaotengenezwa kwa zabibu ni “**Divai**”.

Wakati “Kileo” (Kwa lugha ya kiingereza Beer/Bia) ni kilevi kinachotengenezwa kwa nafaka kama Ngano, mahindi, ulezi, mtama, mchele n.k

Kikawaida Mvinyo ndio wenye kilevi kingi kuliko Kileo. Na matokeo ya mtu anayetumia mvinyo au kileo yanakaribiana. Hebu tuangalia madhara ya kimoja baada ya kingine kibiblia.

## 1. MVINYO

Biblia anasema “**Mvinyo hudhihakiki**”.. maana yake ni kuwa mtu anayetumia mvinyo anakuwa ni mtu wa kudhihakiki na kudhihakikiwa!.. kwasababu ya wingi wa maneno yao yasiyo na maana yatokayo midomoni mwao.

Ndio maana utaona kile kipindi cha Pentekoste, walipowasikia wanafunzi wa Bwana YESU wakinena kwa lugha, walidhani wamelewa kwa mvinyo mpya na hivyo wakaanza kuwadhihakiki..

*Matendo 2:12 “Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, Maana yake nini mambo haya? 13 WENGINE WALIDHIHAKI, WAKISEMA, WAMELEWA KWA MVINYO MPYA.*

*14 Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.*

*15 Sivyoy mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana;*

16 lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli”.

Umeona hapo?.. walianza kuwadhihiki wakidhani wamelewa kwa **MVINYO MPYA**, ikimaanisha kuwa Mvinyo huleta dhihaka kwa anayekunywa. Na mtu anayelewa kwa mvinyo atapokea dhihaka nyingi katika maisha yake..

## 2. KILEO

Biblia inaendelea kusema kileo huleta “UGOMVI”. Asilimia kubwa ya watu wanaogombana mpaka kufikia hatua ya kudhuria ni walevi wa pombe, mafarakano mengi yanatoka kwa watu waliolewa..

Hivyo kwa hitimisho ni kwamba, Ulevi wa aina yoyote ile uwe wa “**Mvinyo**” au wa “**Kileo**” matokeo yake ni mabaya katika maisha ya ulimwengu huu na ule ujao.... Kulingana na biblia walevi wote hawataurithi uzima wa milele (*soma 1Wakorintho 6:9-10 na Wagalatia 5:19-20*)..

*Warumi 13:13 “Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ULAFI NA ULEVI, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu.*

*14 Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake”.*

Maran atha.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Nini maana ya “Mvinyo hudhahaki na kileo huleta ugomvi? (Mithali 20:1)

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

### **Mafundisho mengine:**

#### **UPEPO WA KUSI HULETA MVUA;**

**“Si watu wa kutumia mvinyo sana”, je tunaruhusiwa kutumia mvingo kidogo?(1Timotheo 3:8).**

**Biblia ina maana gani inaposema akonyezaye kwa jicho huleta masikitiko?**

**Je! mwanadamu wa kwanza kuumbwa ni yupi?**

**JE! ULEVI NI DHAMBI?.**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp

Nini maana ya “Mvinyo hudhihakiki na kileo huleta ugomvi? (Mithali  
20:1)

[Print this post](#)